Jarida la wiki
HALMASHAURI YA
JIJI LA DODOMA

# Jiji la Dodoma kinara Michango ALAT



"niishukuru Halmashauri ya Jiji la Dodoma, katika michango ya ALAT Taifa. Halmashauri hii ndiyo inaongoza ulipaji wa michango kwa wakati. Nilipokutana na Waziri wa TAMISEMI nilimshauri kumuacha Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma ili aendelee kutekeleza mipango mizuri aliyonayo kwa Jiji la Dodoma na miradi ya maendeleo"

JUMUIYA ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) imeipongeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa umakini wake katika kuwasilisha michango kwa wakati jambo linaloonesha nia njema na uwajibikaji unaolenga kuifanikisha taasisi hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Murshid Ngeze alipokuwa akiongea katika Mkutano wa mwaka wa ALAT tawi la Mkoa wa Dodoma uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma mwishoni mwa wiki.



*"Mimi na Watumishi wenzangu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma tupo tayari kuhesabiwa. Watanzania wenzangu msikose kuhesabiwa Tarehe 23 Agosti, 2022"*

## Jiji la Dodoma la pongezwa

## Zao la zabibu Dodoma

SIKU 7 ZA JIJI LA DODOMA







# Jiji la Dodoma
## Kinara Michango ALAT Taifa



**MURHID NGEZE**
**Mwenyekiti wa ALAT Taifa**

Na. Dennis Gondwe, DODOMA

JUMUIYA ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) imeipongeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa umakini wake katika kuwasilisha michango kwa wakati jambo linaloonesha nia njema na uwajibikaji unaolenga kuifanikisha taasisi hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Murshid Ngeze alipokuwa akiongea katika Mkutano wa mwaka wa ALAT tawi la Mkoa wa Dodoma uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma mwishoni mwa wiki.

Ngeze alisema "niishukuru Halmashauri ya Jiji la Dodoma, katika michango ya ALAT Taifa. Halmashauri hii ndiyo inaongoza ulipaji wa michango kwa wakati. Nilipokutana na Waziri wa TAMISEMI nilimshauri kumuacha Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma ili aendelee kutekeleza mipango mizuri aliyonayo kwa Jiji la Dodoma na miradi ya maendeleo".

Aidha, aliipongeza ALAT tawi la Mkoa wa Dodoma kwa kazi nzuri. "Sasa umefika wakati ALAT Mkoa wa Dodoma kufikiria kuanzisha miradi ya kiuchumi ili tuache alama. Tufikirie miradi itakayoisaidia ALAT kuwa na mapato ya uhakika na kuachana na kutegemea mapato ya kuombaomba" alisema Ngeze.

Mwenyekiti huyo alielezea masikitiko yake kwenye halmashauri zenye migogoro na kusema kuwa inakwamisha maendeleo ya wananchi. "Mheshimiwa Rais anaona na kusikitishwa na migogoro katika halmashauri. Ameiagiza ALAT kuondoa migogoro hiyo na kuhakikisha halmashauri zinachapa kazi. Hadi sasa kuna halmashauri zipo kwenye migogoro ya kumuondoa Meya na mwenyekiti wa halmashauri, jambo linalochelewesha maendeleo ya wananchi" alisema Ngeze.

Awali akimkaribisha Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Mwenyekiti wa ALAT mkoa wa Dodoma, Zuberi White alisema kuwa ALAT Mkoa wa Dodoma ni wamoja na wanafanya kazi kwa ushirikiano.

Mkutano wa mwaka wa ALAT Mkoa wa Dodoma ulifanyika katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma ukitanguliwa na ziara ya siku moja ya kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa jijini hapo.



**JOSEPH MAFURU**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**

# **WENYEVITI** na wakurugenzi wa halmashauri nchini wametakiwa kuichambua bajeti

WENYEVITI na wakurugenzi wa halmashauri nchini wametakiwa kuichambua bajeti iliyopitishwa na serikali ili wananchi katika ngazi za chini wawe na uelewa na kunufaika nayo.

Agizo hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Murshid Ngeze alipokuwa akiongea katika Mkutano wa mwaka wa ALAT tawi la Mkoa wa Dodoma uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma mwishoni mwa wiki.

Ngeze alisema kuwa serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imepitisha bajeti ya kihistoria na ya mfano. "Ndugu zangu, bajeti hiyo imejaa fursa mbalimbali zenye manufaa kwa halmashauri zetu na wananchi wetu. Wenyeviti wote na wakurugenzi wa halmashauri ni wajibu wenu kuichambua bajeti hiyo na kuwaeleza wananchi ili fedha zitakapokuja kwenye halmashauri zetu ziweze kuwanufaisha na sisi kuzisimamia ipasavyo" alisema Ngeze.

Aidha, aliwataarifu wajumbe kuwa Mkoa wa Kagera umepata shilingi bilioni 70 kwa ajili ya kuanzisha ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba. Alishauri kuwa Mkoa wa Dodoma kujipanga kwa ufugaji huo kutokana na kutokuwa na bahari wala ziwa. Ufugaji huo ni wa kawaida na hauhitaji uwekezaji mkubwa, aliongeza.

Awali akimkaribisha Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Dodoma, Zuberi White alisema kuwa ALAT Mkoa wa Dodoma ni wamoja na wanafanya kazi kwa ushirikiano.
Mkutano wa mwaka wa ALAT Mkoa wa Dodoma ulifanyika katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma ukitanguliwa na ziara ya siku moja ya kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa jijini hapo.



**MURHID NGEZE**
**Mwenyekiti wa ALAT Taifa**



**ZUBERI WHITE**
**Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Dodoma**

# Jiji la Dodoma la pongezwa

## *kwa ujenzi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo*



**MRADI WA GOVERNMENT CITY COMPLEX**

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imepongezwa kwa ujenzi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayolenga kusogeza huduma kwa wananchi na kuongeza mapato.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) Mkoa wa Dodoma, Zuberi White alipokuwa akifungua Mkutano wa mwaka wa ALAT Mkoa wa Dodoma uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma mwishoni mwa wiki.

White alisema kuwa walitembelea miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma na kuridhishwa na utekelezaji wake. "Tumeona wenzetu wanavyotekeleza mradi wa ujenzi wa hoteli ya Dodoma City, ujenzi wa soko la wazi la Machinga, ujenzi wa Kituo cha Afya Chang'ombe, ujenzi wa shule ya mchepuo wa kiingereza, ujenzi wa shule ya sekondari Hombolo Makulu na ujenzi wa jengo la kitega uchumi Mtumba, kwa kweli wenzetu hawa wapo vizuri na wamejipanga sawasawa" alisema White.

Alisema kuwa miradi hiyo ni mizuri. Pamoja na kutoa huduma bora kwa wananchi, miradi hiyo itaongeza mapato ya halmashauri, alisema.

Mkutano wa mwaka wa ALAT Mkoa wa Dodoma ulifanyika katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma ukitanguliwa na ziara ya siku moja ya kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa jijini hapo.






**MRADI WA DODOMA CITY HOTEL**

# **ALAT** ya pongeza Ujenzi wa Soko la Wazi la machinga Dodoma



**MRADI WA SOKO LA WAZI LA MACHINGA DODOMA**

Na. Shaban Ally, Dodoma

Mwenyekiti Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Murshid Ngeze aipongeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kutekeleza mradi mkubwa wa kimkakati wa soko la wazi la Machinga kwa lengo la kuwatengenezea mazingira rafiki ya biashara.

Pongezi hizo alizitoa alipoongoza timu ya ALAT taifa walipofanya ziara ya kutembelea mradi huo uliopo eneo la Bahi road jijini Dodoma.

"Kwa niaba ya ALAT, nikushukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Dodoma pamoja na viongozi wengine wa jiji kwa kuupiga mwingi. Lakini nikuombe mheshimiwa mkuu wa mkoa kuzingatia suala la usalama katika eneo hili la mradi ili kuepusha usumbufu kwa wafanyabiashara", alisema Ngeze.

Ngeze aliushauri uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, kuzingatia maendeleo ya kiuchumi kwa wafanyabiashara hao kwa kuwapa elimu ya biashara ili kuweza kuwakomboa kiuchumi. "Nikuombe mheshimiwa mkuu wa mkoa uweke utaratibu wa mafunzo ya biashara kwa wafanyabiashara hao kwa lengo la kuwaendeleza wafanyabiashara hao" aliongeza Ngeze.

Ngeze alihitimisha kwa kuwaomba viongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma hususani wajumbe wa ALAT, kwenda kujifunza miradi ya maendeleo katika Halmashauri yake ya Kagera ili kupanua mawazo ya kimaendeleo kwa viongozi hao.

Kwa upande wake Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia halmashauri yake kiasi cha shilingi bilioni 2.5 kuendeleza ujenzi wa mradi huo.

Naibu Meya aliwaomba viongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma pamoja na ALAT kudumisha umoja na ushirikiano baina yao ili kuchochea maendeleo zaidi. "Niwaombe ndugu viongozi wenzangu kwa pamoja tudumishe umoja wetu na ushirikiano ili asije akatokea mtu yeyote wa kuvunja umoja wetu", alisema Chibago.







# Zao la zabibu Dodoma

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inaendelea na mageuzi makubwa katika kilimo cha zao la Zabibu ili kiweze kuinua kipato cha wananchi na kukuza pato la taifa.


Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru alipokuwa akichangia katika mkutano wa mwaka wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa halmashauri ya jiji.

Mafuru alisema kuwa halmashauri yake inapambana kuhakikisha zao la Zabibu linazidi kukua. "Zao la Zabibu ni kipaombele chetu, bahati nzuri Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika anafanya kazi nzuri. Tumepeleka wataalam wetu watatu Cape town, Afrika Kusini kujifunza kilimo cha Zabibu. Tumetumia mapato ya ndani kwa wataalam wetu hao kwenda Afrika Kusini kwa siku 10 ili kuleta mapinduzi katika kilimo cha Zabibu" alisema Mafuru.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa katika kuhakikisha zao la Zabibu linashika kasi, alipeleka wachumi kuweka kambi mkoani Morogoro kwa siku 10 kwa ajili ya kuandika maandiko ya miradi ya maendeleo itakayosaidia kukuza zao hilo.



**JOSEPH MAFURU**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**




# SIKU 7

## ZA JIJI LA DODOMA

JARIDA HILI LINATOLEWA NA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

S.L.P 1249 DODOMA, TANZANIA
Baruapepe: cd@dodomacc.go.tz
Tovuti: www.dodomacc.go.tz